

FOCUS A365

Another Manyamfranchise.Com Evaluation Test

FORM 4 TERM 2 KISWAHILI EXAMINATIONS 2018

NAME: _____ ADM NO: _____ CLASS: _____

MATUMIZI YA LUGHA (AL 40)

- (a) Toa mfano wa neno lenye muundo wa silabi ya irabu pekee. (al 1)
- (b) Eleza maana mbili za neno : barabara. (al 2)
- (c) Sahihisha sentensi :
Abiria walisafiri na ndege (al 1)
- (d) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi katika sentensi:
Mwanafunzi mkongwe amepewa tuzo kwa kuwa hodari masomoni. (al 4)
- (e) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi.
Usingeacha masomo, usingetaabika vile. (al 2)

(f) Tunga sentensi ukitumia kielezi cha:

(i) Jumla (al 1)

(ii) Namna linganisho (al 1)

(g) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi :

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo. (al 2)

(h) Eleza maana mbili zinazo patikana katika sentensi:

Nenda ukaniletee mbuzi. (al 2)

(i) Tunga sentensi kudhirisha matumizi ya ngeli ya U-U. (al 2)

(j) Andika katika usemi wa taarifa.

“Mito yetu imechafuka sana; itabidi tuungane mikono wakubwa kwa wadogo, wanaume kwa wanake ili tuisafishe.” Mwanamazingira alituhimiza (al 3)

(k) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale.

Amina na Mustafa huimba taarabu. (al 4)

(l) Eleza matumizi ya ku katika sentensi:

Sikumwelewa alivyoeleza namna ya kuwatunza mbwa wake. (al 1)

(m) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi la katika kauli ya kutendwa. (al 2)

(n) Eleza kazi ya kila kitenzi katika sentensi:

Mkulima angetaka kupalilia shamba lake mapema. (al 4)

(o) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi. (al 4)

(p) Onyesha jinsi moja moja ya matumizi ya viwakifishi vifuatavyo: (al 3)

(i) Nusu koloni (;)

(ii) Herufi kubwa

(iii) Kishangao (!)

1. FASIHI

Kanda la usufi

“Hakujua maisha yangechukua mkondo upi. Mzo wa majuto ulimwandama. Ulimwengu wake umevurugika akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda alijojo.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)

(b) Taja na ueleze tamadthali ya usemi kwenye dondoo hili. (al 4)

(c) Kwa kutolea mifano , onyesha jinsi anwani kanda la usufi inavyoafiki hadithi husika. (al 12)

<http://atikaschool.org>
sales@manyamfranchise.com [0728 450425]

2. Eleza hali ya shaka ya mambo inavyojitokeza katika hadithi ya shaka ya mambo. (al 20)

<http://atikaschool.org>
sales@manyamfranchise.com [0728 450425]